



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAASISI YA UONGOZI



## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI TAASISI YA UONGOZI KUFANYA MAHAFALI YA TISA

**15 Mei 2026, Dar es Salaam:** Sherehe ya mahafali ya tisa ya Taasisi UONGOZI itafanyika leo katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City, Jijini Dar es Salaam. Mgeni Rasmi wa Tukio hili atakuwa Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Wasilisho kuu litatolewa na Mhe. Bal. Dkt. Elsie Kanza, Balozi wa Tanzania nchini Marekani.

Tukio hili linafanyika kwa ajili ya kuwapongeza viongozi waliohitimu programu za mafunzo za muda mrefu: Stashahada ya Uzamili ya Uongozi (*Postgraduate Diploma in Leadership*), Programu ya Uongozi Ngazi ya Cheti (*Certificate in Leadership*), Programu ya Uongozi kwa Wanawake (*Women's Leadership Programme*), na Programu ya Uongozi kwa Viongozi Chipukizi (*Emerging Leaders Programme*). Jumla ya viongozi 231 watahitimu. Aidha, sherehe hii itajumuisha tukio fupi la maadhimisho ya miaka 15 ya Taasisi na uzinduzi wa mpango mkakati wa miaka mitano wa Taasisi (2026/27 – 2030/31). Wageni watakaohudhuria ni pamoja na viongozi waandamizi kutoka nchi mbalimbali barani Afrika – na sekta zote ikiwemo sekta ya umma, sekta binafsi, sekta ya elimu ya juu, na sekta ya asasi za kiraia.

Lengo la programu hizi ni kujenga na kuimarisha uwezo wa viongozi katika maeneo matatu: sifa binafsi za uongozi, usimamizi wa rasilimali watu, na uongozi wa taasisi. Zimeandaliwa kwa ajili ya viongozi wanaotaka kujiendeleza bila kukwamisha kazi yao. Wakufunzi wa programu ni wataalamu wabobezi katika masuala ya uongozi kutoka nchi mbalimbali duniani.

Stashahada ya Uzamili ya Uongozi na Programu ya Uongozi Ngazi ya Cheti zinatolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto cha Mafunzo ya Utawala, kilichopo nchini Finland, Programu ya Viongozi Chipukizi inatolewa kwa kushirikiana na Taasisi ya HAUS ya Mafunzo ya Utawala iliyopo nchini Finland. Utekelezaji wa programu hizi mbili unawezeshwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Finland. Programu ya Uongozi kwa Wanawake inatolewa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Yale cha Mafunzo ya Uongozi kilichopo Marekani, na inafadhiliwa na Serikali hizo mbili pamoja na Umoja wa Ulaya.

Ushiriki katika tukio hili ni kwa mwaliko pekee.

Imetolewa na,

Suzana Aroko

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma**